JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

# SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

[TANGAZO LA SERIKALI NA. 237 LA TAREHE 24/10/2008]

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) (g)*

---

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI, 2008

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za mwaka 2007. Jina

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyomo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika gazeti la Serikali.. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: Tafsiri

"Halmashauri: maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Moshi;

"Mazao" maana yake ni mazao yote ya biashara, mazao ya misitu pamoja na mazao ya chakula ambayo yanatumika katika biashara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayefanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni, shirika, chama cha Ushirika au vikundi vinavyonunua mazao.ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa ajili ya kufanya biashara;

"Mfanyabiashara" katika Sheria Ndogo hizi ni mnunuzi au mkulima anayesafirisha na kuuza mazao yake nje ya Wilaya au anayesindika na kuuza mazao yake yakiwa yamesindikwa;

Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kutekeleza Sheria Ndogo hizi;

"Mtu" maana yake ni mtu asilia au mtu kisheria kama vile kampuni, shirika au jumuiya;

"Ushuru" ni malipo atakayotozwa mnunuzi, mfanyabiashara au mkulima anayesafirisha mazao nje ya Wilaya au anayesindika mazao yake kwa lengo la kufanya biashara;

"Wakala" maana yake ni mtu, shirika au kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kukusanya ushuru wa mazao au mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalosimamia uzalishaji wa shirika, mtu au kampuni nyingine.

Kutoza ushuru

4. -(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa mazao yote ya biashara yanayozalishwa na wenyeji au wawekezaji katika Halmashauri kulingana na viwango vilivyowekwa katika nyongeza "A" ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru wa mazao utakusanywa na wakala au maafisa wa Halmashauri watakaoteuliwa na Mkurugenzi kukusanya ushuru huo.

(3) Ushuru wa mazao utatolewa na kulipwa na mnunuzi au mfanyabiashara kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa katika Sheria Ndogo hizi.

(4) (a) Bila kuathiri maelezo ya kifungu cha 4(3) cha Sheria Ndogo hizi, mkulima anayesafirisha na kuuza mazao yake nje ya Wilaya au anayesindika na kuuza mazao yake yakiwa yamesindikwa na atahesabika kama mfanyabiashara na atatakiwa kulipa ushuru wa mazao kama mnunuzi mwingine yeyote yule;

(b) kiasi cha ushuru utakaolipwa na mkulima anayesindika mazao yake kitahesabika kutokana na kilo, tani au kiasi cha mazao kabla ya kusindikwa kwa mazao hayo.

Mahali pa kulipa Ushuru

5. -(1) Ushuru wa mazao utalipiwa sokoni na kwenye Ofisi za Vituo vya kununulia mazao au katika vituo vya kukagulia mazao ya misitu na mazao ya ndizi yanayosafirishwa kwenda nje ya Halmashauri.

(2) Bila kuathiri maelezo ya kifungu cha 5(1) wakala au Afisa wa Halmashauri atakuwa na haki ya kusimamisha gari lililobeba ndizi mahali popote ndani ya Halmashauri na kulitoza ushuru kama atakuwa na sababu ya kuamini kuwa gari hilo limekwepa kulipa ushuru katika maeneo husika.

(3) Itakuwa halali kwa mnunuzi au mfanyabiashara kuwasilisha na kukabidhi ushuru wake katika Ofisi za Halmashauri zinazohusika.

(4) Ofisi itakayohusika kupokea ushuru wowote wa mazao uliowasilishwa katika Halmashauri ni Ofisi ya kitengo cha mapato katika Idara ya fedha.

(5) Mnunuzi au mtu yeyote atakayelipa ushuru atakuwa na haki kudai na kupewa stakabadhi inayoonyesha kiasi halisi cha ushuru aliolipa.

Taarifa ya mazao yaliyonunuliwa

6. –(1) Mtu, kikundi, Shirika, Chama cha ushirika au Kampuni inayojishughulisha na ununuzi wa mazao italazimika kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusiana na mazao yaliyonunuliwa.

(2) Taarifa inayotakiwa kutolewa kwa Mkurugenzi ni pamoja na takwimu zinazoonyesha idadi ya kilo au tani zilizonunuliwa au kusafirishwa au mazao yaliyosindikwa na bei ya kununulia mazao hayo.

(3) Taarifa zinazotajwa katika kifungu cha 6(1) - (2) cha Sheria Ndogo hizi zinatakiwa zimfikie Mkurugenzi kabla ya tarehe 30 ya kila mwezi.

(4) Maelezo ya kifungu cha 6(1) - (2) cha Sheria Ndogo hizi hata hivyo hayatawahusu wanunuzi wanaonunua mazao sokoni na kuondoka siku hiyo.

(5) Mtu yeyote aliyenunua mazao sokoni atalazimika:–

(a) kutoa takwimu kwa wakala au Afisa wa Halmashauri atakapotakwa kufanya hivyo;

(b) kutoa takwimu kuhusu aina ya mazao, kiasi cha mazao na bei ya kununua yatatakiwa kutolewa kabla ya kusafirisha mazao, wakati wa kusafirisha na katika vituo vya kukaguliwa mazao ya ndizi na misitu.

Mahali na sehemu za kuuza ndizi

7. –(1) Kila mkulima wa zao la ndizi atalazimika kuuza ndizi zilizokomaa.

(2) Ndizi zote zitauzwa katika masoko au magulio yanayotambulika kisheria katika Halmashauri.

Vituo vya ukaguzi

8. –(1) Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi inaanzisha vituo vitakavyotumika kukagua mazao ya misitu na ndizi yatakayosafirishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

(2) Vituo vinavyotajwa katika kifungu cha 8(1) vitafunguliwa sehemu ya njia Panda, Kindi, Kirima, Mamboleo na Mary Benett na vitafanya kazi zake kuanzia saa moja asubuhi hadi saa moja jioni kila siku.

(3) Kila gari linalosafirisha mazao ya misitu na ndizi litalazimika kuingia katika vituo vilivyotajwa katika kifungu cha 8(2) kwa ajili ya ukaguzi.

(4) Dereva wa gari lililobeba mazao ya misitu au ndizi atakayegoma kuingiza gari lake kituoni na kukaguliwa atakuwa ametenda kosa na mzigo wake hautaruhusiwa kuondoka mpaka ametoa faini ya shilingi 25,000/=.

(5) Kila msafirishaji wa ndizi atatakiwa kuonyesha stakabadhi ya ushuru alioulipa sokoni, shambani au sehemu nyingine yoyote alikonunulia ndizi.

(6) Msafirishaji wa ndizi atakayeshindwa kuonyesha stakabadhi ya ushuru aliolipia mazao anayosafirisha atalazimika kulipia mzigo wake katika kituo kulingana na viwango vilivyowekwa katika Sheria Ndogo hizi;

(7) Afisa Muidhiniwa au wakala atakuwa na mamlaka ya kusimamia na kukagua gari linalosafirisha mazao ya misitu au ndizi. Hali kadhalika atakuwa na haki ya kuhoji na kuonyeshwa stakabadhi ya ushuru wa mazao yatakayokuwa yanasafirishwa.

Leseni na kibali

9.–(1) Kila mnunuzi wa mazao ya biashara ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na leseni ya biashara pamoja na kibali toka kwa Halmashauri isipokuwa wanunuzi wa ndizi sokoni au magulioni.

(2) Mfanyabiashara atakayependa kwenda kununua ndizi moja kwa moja toka mashambani kabla hazijapelekwa sokoni itabidi aombe na kupata kibali kama kinavyooneshwa katika nyongeza "A" ya Sheria Ndogo hizi kutoka kwa Mkurugenzi kupitia Afisa Mtendaji wa Kata au kijiji husika.

(3) Itakuwa ni ukiukwaji wa Sheria Ndogo hizi kwa mfanyabiashara kuingia kijijini na kuanza kununua ndizi bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi.

(4) Mkulima wa zao la ndizi atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kama atamuuzia mtu yeyote ndizi bila kuonyeshwa kibali kilichotajwa katika kifungu cha 9(3) cha Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kusafirisha mazao

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza, kununua au kusafirisha mazao kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kabla ya saa 12.00 asubuhi na baada ya saa 12.00 jioni.

11.–(1) Halmashauri itakuwa na nguvu na mamlaka ya kuanzisha vituo vya kuuzia na kununulia ndizi ndani ya Halmashauri kama itaona inafaa na ni lazima kufanya hivyo.

(2) Pale ambapo Halmashauri itakuwa imeanzisha vituo vya kununulia ndizi itaagiza ndizi kutoka vijiji vyote ndani ya Wilaya ziuzwe na kununuliwa katika vituo hivyo.

(3) Mtu atakayekaidi agizo la Halmashauri la kuuza ndizi katika vituo vitakavyokuwa vimeanzishwa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na atalazimika kulipa faini ya Sh. 25,000/=.

12. -(1) Mtu yeyote:

(a) atakayekataa au kusababisha kukataa kulipa ushuru; au

(b) atakayekwepa au atakayesababisha kukwepa kulipa ushuru; au

(c) atakayenunua mazao bila kibali; au

(d) atakayenunua ndizi moja kwa moja kutoka shambani bila kibali; au

(e) atakayekataa kutoa taarifa juu ya tani au kiasi cha mazao aliyonunua au kutoa taarifa za uongo; au

(f) atakayekataa kuingiza gari lake katika vituo vya kukagulia mazao ya ndizi na misitu; au

(g) atakayeuza ndizi changa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

13. -(1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mahakamani atatakiwa kutoa faini isiyopungua Sh. 70,000/= na isiyozidi Sh. 200,000/= au kifungo cha miezi isiyopungua kumi na miwili (12) àu adhabu zote mbili faini na kifungo.

(2) Mkurugenzi atakuwa na mamlaka chini ya Sheria Ndogo hizi kumtoza faini ya papo kwa papo mtu yeyote kama mtu huyo atakiri kosa na kukubali kwa maandishi kuwa yuko tayari kulipa faini hiyo.

NYONGEZA 'A'

KIASI CHA USHURU UNAOTOZWA

| *Na.* | *Aina ya Mazao* | *Kiasi cha Ushuru Unaotozwa* |
|---|---|---|
| 1. | Kahawa | 5% ya bei ya kununulia |
| 2. | Maharage | 3% ya bei ya kununulia |
| 3. | Nyanya | 4% ya bei ya kununulia |
| | Vitunguu | |
| | Viazi | |
| 4. | Mchele | 5% ya bei ya kununulia |
| 5. | Maparachichi | 3% ya bei ya kununulia |

NYONGEZA 'A'

KIASI CHA USHURU UNAOTOZWA

| *Na.* | *Aina ya Mazao* | *Kiasi cha Ushuru Unaotozwa* |
|---|---|---|
| 6. | Ndizi | 5% ya bei ya kununulia |
| 7. | Maua | 5% ya bei ya kununulia |
| 8. | Mahindi | 5% ya bei ya kununulia |
| 9. | Mazao ya Misitu | 5% ya ushuru unaotozwa na mamlaka ya misitu ya Taifa |
| 10. | Miwa | (Forest Royalty) |
| | * | 5% ya bei ya tani 1 ya miwa ambayo haijasindikwa. |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imewekwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la Baraza la Halmashauri lililokutana tarehe 30/3/2007 na imewekwa mbele ya:

ANNAH J. MWAHALENDE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Moshi*

L.S.

STEWART H. LYATUU,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Moshi*

NAKUBALI,

Dodoma,
25 Julai, 2008

MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*